**RULENGE – NGARA CATHOLIC DIOCESE:**

***St. Severine English Medium Boarding And Day Pre And Primary School***

***P.O.BOX 19, BIHARAMULO.***

Website: **www.stseverineschools.ac.tz** Email: st.severineemps@gmail.com


**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2023.**

Wanafunzi wanaohamia wote wanapaswa kufanya mtihani kwanza shuleni na kisha kupewa kibali kutoka kwa Mwalimu Mkuu ili kuthibitishiwa uwepo wa nafasi kwa darasa aliloomba na kutafuta uhamisho. Mitihani hufanyika siku zote za kazi hapa shuleni.

Unapomleta mwanao fika na fomu hii.
(Mzazi unashauriwa kutoa nakala ya fomu hii na kukaa nayo kwa kumbukumbu zako binafsi).

Uongozi wa shule unayo furaha kubwa kumkaribisha mtoto wako mpendwa katika shule yetu , mtoto ambaye umeamua apate elimu bora baadaye.
Shule itafunguliwa tarehe 09 Januari 2023, saa 1:30 asubuhi.

## SHULE MAHALI ILIPO:

Shule imejengwa kilomita 2½ eneo la Rukaragata nje kidogo na mji wa Biharamulo.

## USAFIRI

Shule inaingia makubaliano na wazazi juu ya jinsi ya kuwasafirisha wanafunzi kutoka nyumbani na kuwarudisha wakati wa likizo (mzazi anapaswa kutekeleza wajibu wa kumsafirisha mwanafunzi). Japokuwa wanafunzi wa kutwa husafirishwa kwa gari la shule, hata hivyo ikumbukwe na kufahamika kwamba inapojitokeza kukawepo na tatizo la kiufundi kwenye gari la shule mzazi atajulishwa na hivyo atapaswa kumleta mwanae shuleni na kumfuata jioni ili asipoteze masomo kwa kipindi chote cha tatizo hilo.

## SUALA LA AFYA

Shule imeajiri Mkunga Muuguzi na msaidizi wake kwa ajili ya afya za wanafunzi.
Unashauriwa kumpima mwanao juu ya afya yake na kutoa taarifa sahihi za afya ya mwanao kwa Mwalimu Mkuu ili awapo shuleni apewe huduma kadri ya afya yake, kutotoa taarifa sahihi za mtoto wako shuleni ni dalili za kutompenda na kumtakia MATATIZO ASIYOSTAHILI KUYAPATA. Tunacho kituo cha afya cha Rukaragata, Zahanati ya May Day na Hospitali Teule ya wilaya ya Biharamulo ambazo kwa pamoja hutoa huduma za afya kwa wanafunzi wetu.



Scanned with CamScanner

## MALIPO YA ADA

Fedha zote zitalipwa Bank ya NMB: Jina la akaunti ni: **SCHOOL RULENGE DIOCESE ST. SEVERINE. ACCOUNT NUMBER 31706600027 (Original Pay in slip ndiyo inaletwa hapa shuleni). Isipokuwa malipo ya unifomu yatakuja taslimu ofisini.**

1.1 Malipo ya ada yatakuwa kama ifuatavyo na yatalipwa kwa awamu nne kasoro darasa la saba tu watalipa awamu mbili.

**WANAFUNZI WA KUTWA**

| DARASA | AWAMU I | AWAMU II | AWAMU III | AWAMU IV | JUMLA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|
| AWALI | 195,000/= | 195,000/= | 195,000/= | 195,000/= | 780,000/= |
| PI | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 1,130,000/= |
| PII | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 1,130,000/= |
| PIII | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 282,500/= | 1,130,000/= |

NB: Kwa wanafunzi wa kutwa wanaotumia usafiri watalipa **240,000/=** kwa mwaka ikiwa ni gharama ya usafiri ambayo italipwa kwa awamu nne kila awamu ni sh **60,000/=** tu

### MALIPO MENGINEYO

- Tahadhari kwa wanafunzi wote **10,000/=**
- Huduma ya kwanza kwa wanafunzi wote **10,000/=**
- Kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wasiokuwa na bima ya afya watalipa **50,400/=** kwa ajili ya bima ya afya na waje na picha 'passport size' moja, na kwa wale ambao walishapata bima ya afya watalipia 50,400/= kwa ajili ya kurudia (renew) . (**Tunapokea Bima za NHIF tu kwa wanafunzi wa bweni**).
  **MALIPO YOTE HAYO HUFANYIKA JANUARI TU.**
- 50,000/= kwa kila mzazi kwa ajili ya ujenzi wa darasa inaingia kwenye akaunti ya shule.
  **NB:** Kila mwanafunzi aje na limu mbili aina ya **Double A A4** tutakapo fungua shule Januari na Julai 2023. (Januari 1 na Julai 1).
  **NB:Wanafunzi wote kuanzia darasa la IV mpaka la VII wanatakiwa kuwa bweni.**



Scanned with CamScanner

**KWA WANAFUNZI WA BWENI**

| DARASA | AWAMU I | AWAMU II | AWAMU III | AWAMU IV | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| AWALI | 300,000/= | 300,000/= | 300,000/= | 300,000/= | 1,200,000/= |
| PI | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 1,400,000/= |
| PII | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 1,400,000/= |
| PIII | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 350,000/= | 1,400,000/= |
| PIV | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 1,600,000/= |
| PV | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 1,600,000/= |
| PVI | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 400,000/= | 1,600,000/= |
| PVII | 850,000/= | | 850,000/= | | 1,700,000/= |

**MALIPO MENGINEYO**

- Kwa wanafunzi wa darasa la IV na la VII wanapaswa kulipia malipo ya mtihani kiasi cha sh 80,000/= kwa kila mwanafunzi. Pesa hii italipwa awamu moja tu (JANUARI).
- Tahadhari kwa wanafunzi wote 10,000/=
- Huduma ya kwanza kwa wanafunzi wote 10,000/=
- Kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wasiokuwa na bima ya afya watalipa 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya na waje na picha 'passport size' moja, na kwa wale ambao walishapata bima ya afya watalipia 50,400/= kwa ajili ya kurudia (renew) . (**Tunapokea Bima za NHIF tu kwa wanafunzi wa bweni**).
- 50,000/= kwa kila mzazi kwa ajili ya ujenzi wa darasa inaingia kwenye akaunti ya shule.
  **NB:** Kila mwanafunzi aje na limu mbili aina ya **Double A A4** tutakapo fungua shule Januari na Julai 2023. (Januari 1 na Julai 1).

  **NB:Wanafunzi wote kuanzia darasa la IV mpaka la VII wanatakiwa kuwa bweni.**



Scanned with CamScanner

## 1.1 MAHITAJI YA MWANAFUNZI WA KUTWA WAKATI WA KUFUNGUA

1. Jezi ya mpira (kaptura na T-shirt) wavulana rangi ya bluu na wasichana rangi nyekundu.
2. Faili (aina ya Box File) moja.
3. Shilingi 100,000/= kwa ajili ya sare za shule ambazo ni kaptura/sketi 2, sweta 2, T-shirt 1, Soksi pair 2 na shati 2.Malipo hayo yanalipwa taslimu ofisini.
4. Wanafunzi wa darasa la tatu waje na counter books 12 quire 2 na madaftari madogo ya kati 12 kalamu watapewa shuleni. Darasa la awali na la pili watapewa madaftari na kalamu shuleni.
5. Aje na photocopy ya cheti cha kuzaliwa (birth certificate) pamoja na photocopy ya kitambulisho cha utaifa (National Identity) cha wazazi wa mtoto.

## 1.1.MAHITAJI YA MWANAFUNZI WA BWENI WAKATI WA KUFUNGUA.

Mwanafunzi atakuja shuleni na vifaa vifuatavyo;-

1. Aje na godoro la Dodoma au Super Banco futi 2½ kwa 6 lililofunikwa kwa PVC, Blanket ndogo 1 pamoja na chandarua ya pembe nne rangi nyeupe.
2. Mashuka manne (4) rangi ya light bluu kwa wavulana na rangi ya pink kwa wasichana, Taulo 1 na ndoo ndogo ya plastiki 1.
3. Mavazi ya usiku Track Suit pea moja rangi ya bluu kwa wavulana na nyekundu kwa wasichana, leso 3, chupi 6, kwaruzo kwa ajili ya kuchana nywele, viatu vya ngozi pea 2, viatu vya michezo pea 1 pamoja na soksi za michezo.
4. Sanduku 1 la mbao/chuma imara lenye kufuri kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.
5. Mafuta ya kujipakaa anayotumia mwanao chupa kubwa mbili za gram 500 kila moja.
6. Jezi ya mpira (kaptura na T-Shirt) rangi ya bluu kwa wavulana na nyekundu kwa wasichana.
7. Dawa ya meno tyubu mbili za gram 80 kila moja na miswaki 3.
8. Faili (aina ya Box file) moja.
9. Dawa ya viatu na brashi kadri ya matumizi ya mwanao zisipungue mikebe miwili.
10. Shilingi 120,000/= kwa ajili ya sare za shule na za kushindia ambazo ni kaptura/gauni 4, sweta 2, T-shirt 1, Soksi pair 2 na shati pair 4.Malipo hayo yanalipwa taslimu ofisini.
11. Aje na photocopy ya cheti cha kuzaliwa (birth certificate) pamoja na photocopy ya kitambulisho cha utaifa (National Identity) cha wazazi wa mtoto.
12. Watoto wote waje na yeboyebo pea 2.
13. Wanafunzi waje na madaftari darasa la tatu hadi darasa la saba waje na counter books 12 quire 2 na madaftari madogo ya kati 12 kalamu watapewa shuleni. Darasa la awali na la pili watapewa madaftari na kalamu shuleni.



Scanned with CamScanner

**MUHIMU:** (Hakikisha vifaa vyote umeandika majina ya mtoto kwa kutumia rangi au kufumwa). Vifaa kama sare, blanketi, mashuka, taulo na sanduku viwekwe alama ya maandishi ya jina la mtoto kwa kufumwa au kutumia maandishi ya rangi. Pia mtoto aje na nguo chache za kutumia wakati anasubiri sare za shule.

## KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

1. Taaluma:

   Lengo kuu la shule yetu ni kuandaa wanafunzi wawe na ufaulu mzuri hivyo basi mvivu na mzembe hatadumu hapa shuleni. Kwa mantiki hiyo tutamshauri mzazi kumtafutia mwanae shule nyingine inayokubaliana na uzembe binafsi wa mwanafunzi.

2. **NIDHAMU**

   Hii ni taasisi ya elimu iliyo chini ya Kanisa Katoliki, hivyo wanapewa na kufundishwa maadili mema yanayompendeza Mungu. Utovu wowote wa nidhamu unaadhibiwa mara unapojitokeza hapa shuleni. Aidha kwetu adhabu ya viboko kwa watoto watukutu haiepukiki.

   **NB:** Hii ni shule inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge-Ngara hivyo mwanao kwa kipindi chote atakachokuwa hapa shuleni atalelewa katika maadili ya Kanisa Katoliki si kwamba tutambadilisha dini yake isipokuwa atapaswa kuzijua tunu za Kanisa ambamo anapatia elimu, hivyo atapaswa kuhudhuria matukio yote yanayoendana na Kanisa Katoliki.

Ndugu mzazi kama umesoma na kuelewa maelezo haya uongozi wa shule unakuomba ushirikiano wako katika kuzingatia mtoto na taratibu za shule kwa kuweka saini yako.

Mimi (Jina)________________________________________

Mzazi/Mlezi wa ____________________________________

Nimesoma na kuelewa haya na ninaahidi kutoa ushirikiano wa kustosha.

Saini:……………………………. Tarehe:………………………..

Tunakutakia maandalizi mema.

**NB:** Fomu hii inarudishwa shuleni siku ya kumleta mtoto ambapo atapokelewa na Mwalimu Mkuu kwa ajili ya usajili.

Imesainiwa na;

……………..!.

Theodor Rugendo

M/ MKUU.

ST. SEVERINE PRE & PRIMARY SCHOOLS
THE HEADTEACHER
P. O. Box 19
BIHARAMULO

Scanned with CamScanner